



Atakayependa Mwenyezi Mungu amuokoe na Matatizo ya siku ya Kiyama, basi amtatulia shida mwenye hali ngumu au ampunguzie

Kutoka kwa Abuu Qatada radhi za Allah ziwe juu yake yakwamba yeye siku moja alimtafuta mdai wake, akajificha, kisha akampata, akasema: Hakika mimi nina hali ngumu, akasema: Je, unamuapa Mwenyezi Mungu juu ya hilo? Akasema: Ndio, ninamuapa Mwenyezi Mungu juu ya hilo. Akasema: Kwani mimi nilimsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake akisema: "Atakayependa Mwenyezi Mungu amuokoe na Matatizo ya siku ya Kiyama, basi amtatulia shida mwenye hali ngumu au ampunguzie".

[Sahihi] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Abuu Qatada Al-Answari radhi za Allah ziwe juu yake alikuwa akimtafuta mdaiwa wake aliyekuwa akijificha, akampata, mdaiwa akasema: Mimi nina hali ngumu, na sina mali ya kulipa deni lako. Abuu Qatada radhi za Allah ziwe juu yake akamtaka aape kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa hana mali? Akaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa ni mkweli katika hayo anayoyasema. Akasema Abuu Qatada radhi za Allah ziwe juu yake kuwa yeye alimsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake akisema: Atakayependezwa na akafurahishwa kuwa Mwenyezi Mungu amuokoe na misukosuko ya siku ya Kiyama na matatizo yake na vitisho vyake, basi amtatulia shida mwenye hali ngumu, kwa kumpa muda mrefu na acheleweshe kumdai deni lake, au apunguze sehemu ya deni au amsamehe deni lote.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/4195>

